

Mtazamo Wa Qur'an Juu Ya Kutabaruku

Katika Qur'an tunatosheka na aya moja tu, nayo ni ile inayomnukuu Nabii Yusuf [a] akisema:

"Nendeni na kanzu yangu hii mukaiweke usoni kwa baba yangu (macho yake yatarudi) ataona."

Qur'an, 12:93.

Nabii Yusuf aliituma kanzu yake kwenda kwa baba yake na akawaambia ndugu zake "Nendeni na kanzu yangu hii na muiweke usoni kwa baba yangu ili macho yake yarudi apate kuona.

Mwenyezi Mungu anasema: **"Na alipokuja mtoaji habari njema, aliweka kanzu ile usoni kwake na macho yalirudi akaona."** Qur'an, 12:96.

Aya hii iko wazi kutoa ruhusa ya kutabaruku kwa athari za Manabii na Mawalii kiasi kwamba hata Nabii anataruku kwa Nabii mwenziwe kama hivi Nabii Yaqub [a] anataruku kwa kanzu ya Nabii Yusuf [a].

Na ni wazi kabisa kwamba kuponya kunatoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na yeye ndiye mtendaji halisi, isipokuwa kutabaruku kwa kanzu ya Nabii kumekuwa ni wasila wa kuponya kama tunavyotumia dawa kuwa ni wasila wa kupona kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ewe msomaji ingekuwaje kama kutabaruku kwa Nabii Yaqub kwa kanzu ya mwanawe Yusuf kungelitokea mbele ya watu wa Najdi na wafuasi wa Muhammad Ibn Abdul-Wahab, wangelihukumu namna gani jambo hili?

Je, wangehukumu kuwa ni kafiri au mshirikina au mwenye dhambi? Wakati yeye ni Nabii na ni Ma'asum?

Kutabaruku kwa Waislamu kwenye kaburi la Mtume [s] na makaburi ya watu wa nyumba yake na pia athari zao hakuna tofauti na kutabaruku alikotabaruku Nabii Ya'qub [a] kwa kanzu ya mwanawe Yusuf [a].

<https://www.al-islam.org/uchunguzi-juu-ya-uwahhabi-ayatullah-jafar-subhani/mtazamo-wa-quran-juu-ya-kutabaruku#comment-0>